**KAULI YA AWALI YA SERIKALI BUNGENI KUHUSU MLIPUKO ULIOTOKEA KATIKA MKUTANO WA HADHARA WA KAMPENI ZA UCHAGUZI KATIKA KATA YA SOWETO JIJINI ARUSHA TAREHE 15/6/2013**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, Naomba kuwasilisha Taarifa ya awali kuhusu tukio la mlipuko uliotokea kwenye Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi wa Chama cha CHADEMA katika Kata ya Soweto Jijini Arusha tarehe 15/6/2013 saa 12 jioni.

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 15/6/2013 ilikuwa siku ya kuhitimisha Kampeni za Uchaguzi wa Madiwani katika Kata 26 katika Nchi yetu. Katika Jiji la Arusha kulikuwa na Mikutano mitatu iliyohusisha vyama vitatu vya siasa CCM, CHADEMA na CUF. Mikutano hiyo ilihudhuriwa na mamia ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Ilikuwa ni katika mkutano wa Chama cha CHADEMA, uliofanyika katika Kata ya Soweto ambapo baada ya hotuba za Kampeni kumalizika, Viongozi wa Chama hicho walianzisha harambee ya kuchangia Chama chao. Wakati zoezi hili likiendelea, mtu asiyejulikana alirusha kitu katika kundi la watu kilichosababisha mlipuko mkubwa na taharuki kubwa miongoni mwa wananchi waliokusanyika.

**Mheshimiwa Spika**, Mkutano huu ulikuwa na ulinzi wa Jeshi la Polisi wakiwa na magari mawili na Askari walisimama upanda wa Kaskazini ya

Uwanja na mrushaji wa mlipuko huo alikuwa upande wa Mashariki ya uwanja huo na akarusha kuelekea Magharibi. Jaribio la Askari wa Polisi kutaka kumfuata aliyerusha mlipuko huo zilizuiliwa na makundi ya wananchi ambao walianza kuwashambulia Polisi kwa mawe na kuwazomea na hivyo Polisi kulazimika kuanza kujiokoa badala ya kumsaka mhalifu huyo.

**Mheshimiwa Spika,** Mlipuko huo ulisababisha watu wawili kufariki dunia ambao ni Judith Wiliam mwenye umri wa miaka 48 na mtoto Ramadhani Juma mwenye umri wa miaka 15. Watu 70 walijeruhiwa miongoni mwao watatu walijeruhiwa vibaya na wawili hali zao ni mbaya.

**Mheshimiwa Spika**, Mara baada ya tukio hilo Kamanda wa Polisi Mkoa, Mkuu wa Polisi Wilaya na Timu ya Wapelelezi walifika eneo la tukio kufanya upelelezi wa awali ikiwa ni pamoja na kukagua eneo la tukio, kufanya mahojiano na baadhi ya mashuhuda, kudhibiti eneo la tukio pamoja na kutoa msaada wa majeruhi na kuwapeleka hospitalini. Katika uchunguzi wa awali umeonyesha kuwa mlipuko huo ulikuwa ni wa bomu la kurushwa kwa mkono (hand grenade) ambalo lilirushwa kutoka upande wa Mashariki kuelekea Magharibi kulikokuwa na gari aina ya Fuso lililokuwa linatumika kuhutubia.

**Mheshimiwa Spika**, Aina ya urushaji wa bomu hilo, hautofautiani na mbinu iliyotumika kwenye shambulio lingine la bomu lililotokea tarehe 5 Mei, 2013 katika Kanisa Katoliki la Olasiti katika Jiji hilo hilo la Arusha .

**Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Polisi lina wajibu wa Kisheria na Kikatiba wa kulinda watu na mali zao. Na wanapokuwepo kwenye mikutano ya hadhara ya kijamii au ya kisiasa, wanakuwa pale ili kuwalinda raia, wanaaga familia zao kuwa wanakwenda kazini kuwalinda Raia na mali zao, hivyo ni muhimu Raia kujua kuwa Polisi wapo kwa ajili yao. Kwa miaka mingi Raia wamekuwa wakijua wajibu wa Polisi, ndio maana wanapotafuta haki, wakiuawa wafiwa wanatoa taarifa Polisi, wakiibiwa wanatoa taarifa Polisi, wakipigwa wanatoa taarifa Polisi na hata wakitukanwa wanatoa taarifa Polisi kwa kuwa wanajua Polisi ni chombo chao cha awali katika kutafuta haki.

**Mheshimiwa Spika**, Siku za hivi karibuni, zimekuwepo jitihada za makusudi za baadhi ya vyama vya siasa, makundi ya Kijamii na watu binafsi kupandikiza chuki ya Raia dhidi ya vijana wetu wa Jeshi la Polisi, kuwafanya Raia wawachukie Askari, kuwafanya Raia wasiwaamini Askari, kuwafanya Raia wasiwape ushirikano Askari na hatimaye kuwa na Taifa ambalo halitawaliki.

**Mheshimiwa Spika**, Askari wetu hawa ni wale ambao wanajitolea usiku na mchana ili Watanzania wenzao wawe salama. Hawa ni Askari ambao wanauwa kila siku na majambazi wakiwa wanatutetea, hawa ni Askari ambao ni watoto wa Taifa hili nao ni Watanzania wanaofanya kazi za hatari kwa ajili yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Kufanikiwa kutoroka kwa mharifu wa Soweto ni matokeo ya uchochezi unaofanywa kwa makusudi na baadhi ya wanasiasa

dhidi ya Serikali na Polisi na hivyo kuwafanya wananchi wajenge chuki dhidi ya polisi. Na kutokana na wananchi kujazwa chuki, ndiyo ikatokea badala la kuwapa ushirikiano Polisi waliokuwa pale kuwalinda wao walianza kuwashambulia. Hatimaye badala ya kumsaka mhalifu wakaanza kupambana huku wananchi wanashambulia na Askari wanajihami.

Sote tunajiuliza kwa nini wananchi waliwashambulia na kuwazuia askari wasitimize wajibu wao? badala ya kuwasaidia ili wamkamate mhalifu? Je ilitokea kwa bahati mbaya au ilipangwa?

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 6 Mei, 2013 Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alipotoa taarifa ya Serikali juu ya shambulio la bomu la Olasiti alisema, Nanukuu;

***"Siku za hivi karibuni, zimekuwepo jitihada kubwa sana za watu wachache wasioitakia mema Nchi yetu kutaka kupandikiza chuki za kidini miongoni mwa Watanzania na kuleta mapigano na mauaji miongoni mwa Watanzania. Sina shaka kuwa shambulio la Arusha ni sehemu ya mikakati hiyo miovu".*** Mwisho wa kunukuu.

**Mheshimiwa Spika**, Shambulio la Soweto limehama toka kanisani sasa wamehamia kwenye mikutano ya kisiasa. Nia ni ile ile ya kuwafanya Watanzania wachukiane, wapigane na Taifa letu liparanganyike. Baadhi ya wanasiasa ama kwa bahati mbaya ama kwa kujua na kushiriki mpango huo wamekuwa wakitoa kauli mfululizo za kuendeleza chuki za kijamii wakidhani wanajimarisha kisiasa kumbe wanapanda mbegu ya uharibifu

kwa Taifa letu, mbegu itakayozaa chuki, vita na majuto makubwa ikiachwa iendelee.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uzito na umuhimu wa kuharakisha uchunguzi huu Jeshi la Polisi limeunda timu ya Maafisa Upelelezi itakayoongozwa na Mkuu wa Operation wa Jeshi la Polisi, Kamishna Paul Chagonja. Timu hii itashirikisha pia Vikosi vyote vya Ulinzi na Usalama likiwemo Jeshi la Ulinzi la Wananchi (JWTZ).

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imepania kuwasaka na kuwatia mbaroni wahusika wa shambulio hilo la watu waoga na waovu. Kupitia Bunge hili nataka niwaambie wahalifu hao kuwa njama zao za kutugawa kwa misingi ya Dini, Makabila, Rangi, Rasilimali na Itikadi za Vyama **ZITASHINDWA.** Tutapambana nao usiku na mchana, kwa silaha zote tulizonazo mpaka tutakapo washinda na kuwafikisha mbele ya mikono ya Sheria .

**Mheshimiwa Spika,** Naowaomba Watanzania kote Nchini kuungana na Serikali yao kuwasaka wahalifu hao.

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 1978 Nduli Idi Amini alishambulia Kagera, Watanzani wote tuliungana, wengine walikwenda mstari wa mbele, wengine walichanga fedha, wengine walichanga mifugo, wengine walichanga damu, wengine waliomba dua ilimradi kila Mtanzania alipambana mpaka tukashinda uvamizi ule.

**Mheshimiwa Spika,** Adui wa sasa ni mbaya zaidi maana anataka kutupiganisha wenyewe kwa wenyewe, aivunje vunje nchi yetu kwa kutumia mikono yetu. Alipotangaza vita Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alisema, nanukuu;
***"Nia ya kumpiga tunayo, Sababu za kumpiga tunazo na Uwezo wa kumpiga tunao".*** Mwisho wa kunukuu.

Leo Watanzania wote, wa dini zote, wa makabila yote, wa vyama vyote vya siasa turejee maneno ya Mwalimu kwa kauli na vitendo. Tuwakemee na kuwakabili maadui hawa, wawe wa ndani au wa nje na tuape kuilinda na kuitetea nchi yetu. Tuape kuendeleza Upendo, Umoja na Mshikamano wa Watanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Nimalizie kwa kuwapa pole ndugu na jamaa wa marehemu, Mwenyezi Mungu azilaze mahala pema peponi roho zao. Tunawaombea majeruhi Mungu awape nafuu wapone haraka. Nawapa pole wananchi wa Soweto na Arusha na kuwaomba wazikatae propaganda zote zenye sura ya uchochezi na uongo zinazoenezwa kwa makusudi na baadhi ya watu na wanasiasa wenye nia mbaya. Kwanini Arusha iliyokuwa na amani, upendo na iliyotulia sasa panakuwa mahali pa hofu na mvurugano mkubwa? Kulikoni?

Sote tushirikiane kuikataa hali hiyo isiendelee Arusha na mahali pengine popote Nchini mwetu. Tanzania ni yetu sote, ikiharibika sote tumeharibikiwa! Wote tuseme basi inatosha na tushirikiane kupambana na maovu haya.

**Mwisho:** Serikali imetenga shilingi milioni 100 kama zawadi kwa watu watakaotoa taarifa zitakazofanikisha kunaswa kwa mhalifu wa matukio ya aina hii na mtandao wake. Kila mwananchi atakayetoa taarifa sahihi atapewa milioni 10 na atahakikishiwa ulinzi wa maisha yake. Endapo zitatolewa taarifa sahihi kuhusiana na uharifu huo na fedha zilizotengwa za milioni 100 kuisha, Serikali ipo tayari kuongeza fedha nyingine.

**Mheshimiwa Spika**, Nakushukuru kwa kunipa fursa hii, nawashukuru kwa kunisikiliza.

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika

Naomba kuwasilisha.